**BARAZA LA VYAMA VYA SIASA**

**TAARIFA YA BARAZA LA VYAMA VYA SIASA KWA UMMA KUHUSU KIKAO CHA BARAZA LA VYAMA VYA SIASA KILICHOFANYIKA TAREHE 12 NA 13 MACHI 2025**

## 1.0 UTANGULIZI

Baraza la Vyama vya Siasa limefanya kikao cha kawaida tarehe 12 na 13 Machi 2025 katika Hoteli ya Nashera Morogoro. Katika kikao hicho ajenda zifuatazo ziliwasilishwa;

1. Mafanikio na changamoto za Baraza la Vyama vya Siasa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita; na
2. Kuvijengea uwezo Vyama vya Siasa kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kikamilifu.

Vilevile, masuala yafuatayo yaliwasilishwa na kujadiliwa.

1. Mradi wa kutoa elimu kwa viongozi wa Vyama vya Siasa kuhusu Sheria zinazosimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; na
2. Mradi wa kutoa elimu kwa viongozi wa Vyama vya Siasa kuhusu nafasi ya Watu Wenye Ulemavu katika siasa na uongozi.

## 2.0 MAAZIMIO

Baada ya majadiliano wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa waliazimia yafuatayo:

1. Baraza la Vyama vya Siasa linatumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada anazochukua za kutetea haki za Wanawake na kuwapa Wanawake fursa za kiuchumi, kielimu na uongozi. Baraza la Vyama vya Siasa linatoa shukrani na pongezi hizo kwa sababu, tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani fursa za kiuchumi, kielimu na uongozi kwa Wanawake zimeongezeka kwa kiasi kikubwa. Vilevile, mifumo ya kulinda haki za Wanawake imeimarika na elimu kuhusu haki za Wanawake na masuala ya jinsia inawafikia Watanzania wengi.
2. Baraza la Vyama vya Siasa pia linawapongeza wanawake wote nchini kwa kuazimisha miaka 30 ya mkutano wa Beijing. Vilevile linaipongeza

Serikali kwa mafanikio yaliyopatikana ya kulinda haki za Wanawake tangu mkutano wa Beijing hadi sasa. Baraza litaendelea kuheshimu haki za Wanawake ikiwemo haki ya kushiriki katika siasa na uongozi. Baraza la Vyama vya Siasa linatumia fursa hii pia kuviasa Vyama vya Siasa kuwa na programu maalumu ya kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu kuweza kushiriki katika shughuli za Siasa na kuwa viongozi.

3. Aidha, katika kipindi hiki tunapoelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, Baraza la Vyama vya Siasa linakemea wanasiasa wanaotumia vibaya majukwaa ya kisiasa kwa kuhamasisha uvinjifu wa Katiba na Sheria za nchi na ukiukwaji wa maadili ya kitanzania. Hivyo, Baraza la Vyama vya Siasa linaviasa Vyama vya Siasa kuheshimu Katiba, Sheria za nchi, maadili ya vyama vya siasa, maadili ya uchaguzi na maadili mengine nchini, ili kudumisha Amani, Utulivu na Umoja wa kitaifa katika kipindi chote cha uchaguzi.

..........................................

Mheshimiwa Juma Ali Khatib

**MWENYEKITI BARAZA LA VYAMA VYA SIASA**

13 Machi 2025